

Mafumbo ya Mwanamke katika Mashairi Teule ya Muyaka

Author

Sheila Pamela Wandera- Simwa 

Email: sheiwande@gmail.com

Laikipia University, Kenya.

Cite this article in APA

Wandera- Simwa, S. P. (2022). Mafumbo ya mwanamke katika mashairi teule ya Muyaka. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 1(1) 50-68. <https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.245>



A publication of Editon
Consortium Publishing (online)

Article history

Received: 08.05.2022

Accepted: 30.07.2022

Published: 31.08.2022

Scan this QR to read the paper online



Copyright: ©2022 by the author(s).
This article is an Open Access article
distributed under the terms and
conditions of the Creative Commons
Attribution-NonCommercial-
ShareAlike 4.0 International License
(CC BY-NC-SA 4.0).



Ikisiri

Azma kuu ya makala hii ni kuchanganua mafumbo ya mwanamke wa Kiswahili wa karne ya kumi na tisa katika ushairi wa Kiswahili wa kipindi hicho. Kwa kutumia mashairi teule ya Muyaka, sura ya mwanamke huyo inabainishwa. Mwandishi anaongozwa na nadharia ya uhalisia hasa mhimili wa lugha unaosisitiza kuwa lugha sharti iambatane na wakati wake ili iweze kueleweka na wasemaji wake kimuktadha na kimatumizi. Mbali na kudurusu makala muhimu maktabani, mtafiti kwa kuelekezwa, alikwenda nyanjani kuwahoji Waswahili kuhusu utamaduni wao, hususan ule wa karne ya kumi na tisa. Katika makala hii, imedhihirika wazi kwamba, picha ya mwanamke wa Kiswahili inayochorwa katika mashairi teule ya Muyaka ina misingi yake katika utamaduni wa Waswahili wa karne hiyo. Makala hii itasaidia katika kueleweshwa picha ya mwanamke wa Kiswahili wa karne ya kumi na tisa kama alivyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili wa karne hiyo.

Maneno muhimu: Mafumbo, uhalisia, utamaduni, shairi.

UTANGULIZI

Makala hii inachanganua mafumbo ya mwanamke wa Kiswahili kama yanavyojitokeza katika mashairi teule ya Muyaka, ya karne ya kumi na tisa. Kinachozingatiwa sana katika makala hii ni kujaribu kuonyesha namna utamaduni wa Kiswahili unavyobainika kupitia istilahi za mafumbo hayo. Mashairi yaliyoteuliwa ni: 'Kimbiji Changu', 'Siupati Usingizi', 'Nazi na maji Si mbata', 'Utavaa Nguo gani?' na 'Kuonana na wewe'. Mashairi haya yamedondolewa kutoka kitabu cha Abdullaziz (1979). Katika kuhakiki picha hii, maisha ya Muyaka yamegusiwa kwa kifupi ili kuyapa mashairi teule muhtadha mahsusi. Hii ni kwa sababu msanii, kama mwanajamii, huandika kutokana na tajriba za kimaisha anazozipata kutoka kwa jamii anamoishi. Ndio maana maandishi mengi yanayoandikwa huwa yanahusu msanii mwenyewe, jamii yake, na wakati (kipindi) fulani katika historia. Haya yanazungumziwa na Magayu (1977) anaposema:

Fasihi ni kielelezo cha hali ya maisha. Kama kioo, mara nyingi huwa inamulika sehemu fulani ya Maisha ya mtu binafsi au kundi la watu na uhusiano wao na mazingira yao.

Kutokana na kauli hii, inaaminiwa kuwa mtunzi huyu anaelezea kuhusu jamii yake kwa uhalisi wa mambo yalivyokuwa katika kipindi cha karne ya kumi na tisa. Kwa hivyo, mengi kuhusu maisha ya Muyaka yanatarajiwa kupatikana kwa kudadisi tungo zake.

MAPITIO YA MAANDISHI

Maisha ya Muyaka hayajashughulikiwa kwa kina, hali inayomfanya mtafiti kurejelea takriban mashairi yake yote yaliyokusanywa ili kuweza kuibuka na hoja mwafaka kuhusu maisha ya mshairi huyu. Kwa mwelekeo huu, utafiti huu hautazingatia mashairi hayo matano yaliyoteuliwa peke yake kutoa kauli kuhusu maisha ya Muyaka. Kufanya hivyo ni kujipa uwanja finyu mno wa kuweza kukata kauli yoyote ile kuhusu maisha ya muyaka. Hii ni kwa sababu Muyaka, tofauti na washairi wengine wa wakati wake, yeye ametunga mashairi mengi yenye maudhi tofauti tofauti, kiasi cha kudaiwa kuwa aliuondoa ushairi wa Waswahili msikitini na kupeleka sokoni (Abdullaziz, 1979).

Kwa mujibu wa maelezo ya mwalimu sikujua na Robert Taylor wakinukuliwa katika kitabu cha William Hichens

cha *Diwani ya muyaka* (1940) Muyaka bin haji Al Ghassany alizaliwa katika sehemu ya mji wa kale huko Mombasa mwaka wa 1776 (Abdullaziz, 1979:107). Ingawa kwingineko imedaiwa kuwa Muyaka alikuwa mmoja wa watu wa mlango wa Banu Ghassan (kundi lililotoka Syria), Abdullaziz (1979:107), anatoa tahadhari ya kuikubali kalima hii moja kwa moja. Hii ni kwa sababu, kundi la Ghassani la kutoka Omani halihusiki na Muyaka kwa vyovyote vile. Abdullaziz anaelezea kuwa, ikiwa ni kweli kwamba uhusiano upo baina ya Muyaka na Waghassani wengine, ingekuwa rahisi kuufuata uhusiano huo wa kifamilia kwa vile wengi wa waarabu wa Omani wanazingatia sana jambo la ukoo. Kwa maoni ya Abdullaziz kuhusishwa kwa Muyaka na asili ya kiarabu huenda kumetokea wakati ambapo ubaguzi wa Waswahili kwa misingi ya uwenyeji wao uliwafanya wengi wajipatie majina ya nasaba za watawala wa Kiomani ili angalau wafaidike. Kwa hivyo, ikiwa asili hiyo ipo, huenda ni ya kitambo cha mababu zake. Muyaka alipozaliwa hakuwa na uhusiano wowote wa karibu na hao Waghassani wa Uarabuni. Uswahili wa Muyaka unajitokeza bayana anapotajwa na Taylor kwa jina halisi la Waswahili, Muyaka bin Mwinyi Haji (Abdullaziz, 1979:108). Muyaka alikuwa mmoja wa Waswahili wa mlango wa Mwinyi Malindi kama inavyoelezwa katika kitabu cha *Diwani ya Muyaka*.

Katika maisha yake, pamoja na kuwa mshairi hodari, Muyaka alikuwa mwana biashara. Alifanya biashara kwa kusafiri hadi sehemu mbali mbali ikiwemo miji ya Aden, Muscat, visiwa vya komoro, miji kadhaa ya hindi na huko Shamu (Abdullaziz, 1979:109). Mojawapo wa bidhaa walizoshughulikia ni mtama, ambao inadaiwa alisafiri mara kwa mara hadi sehemu za Lamu kuununua (Abdullaziz 1979:109). Wakati Muyaka akijishughulisha na biashara, mji wa Mombasa ulikuwa ukijulikana kwa biashara za bidhaa kama vile pembe za ndovu na za vifarua, chuma, tumbaku, mikeka, kamba na mifugo (Abdullaziz, 1979:43). Inakisiwa kwamba huenda Muyaka pia aliua bidhaa za aina nyingine pamwe na mtama.

Licha ya kufanya biashara ambayo ilimfikisha kwingi, imedaiwa kuwa Muyaka hakuwa na mali nyingi. Jambo hili linajitokeza katika mashairi yake anapolalamikia mavazi yake yaliyochakaa. Anasema haya kuhusu mavazi:

Natamani kulivuta, tao la nyanje
maua;
Kulla ambapo napita, haoneka na
sitawa;
Sio hofu tupa ukuta, tangu chambwa
na kuambiwa,
Nna ukunyunywa wa t'awa, na
kujikuna nguoni
(Abdullaziz, 1979: 109).

Malalamiko haya ya Muyaka yanaonyesha hali ya maisha anayoishi Muyaka. Anatamani kuyageuza maisha haya kwa mavazi mazuri ili apate kuonekana kama mtu mwenye mali na anayemudu maisha bila kutoa jasho jingi. Katika mshororo wa mwisho wa shairi hilo, Muyaka anaelezea kuwa nguo zake zimejaa chawa ambao wanamfanya ajikune. Hii ni ishara ya umaskini! Ikiwa kauli hii ina ukweli, basi, hapana shaka kwa Muyaka alikuwa mwenyeji wa sehemu ya mji wa kale inayodaiwa kwamba ilikuwa na majengo mabovu na makuuku inapolinganishwa na sehemu ya Gavana wakati huo. Gullian (1846), akinukuliwa na Abdullaziz (1979:14), ameeleza yafuatayo kuhusu majengo ya sehemu za mji wa kale, na ya Gavana. katika kipindi cha katikati mwa karne ya kumi na tisa:

Sehemu moja ya mji imejengwa
nyumba za mawe zenye gorofa moja
na zina roshani [balchony]. Sehemu
ile nyingine imejengwa vibanda
vilivyozekwa kwa nyasi [makuti]
mithili ya ulivyo mji wa Zanzibari ...

Habari kumhusu Muyaka kama mume na mzazi, kama ilivyo kuhusu mambo yake mengine, ni haba. Kuna habari kuwa, mtoto wake aliyetwa Ali wa Muyaka alipata kuonekana na mzee mmoja wa Mombasa aliyetwa Sheikh Ahmed Bin Tahir. Mzee huyu aliaga dunia mwaka wa 1948 (Abdulaziz, 1979: 107). Hakuna ripoti yoyote nyingine inayojulikana kuhusu watoto wa Muyaka. Ingawa inasemekana Muyaka alikuwa na wake watatu (Imbosa, 1990) ni jina la mke mmoja tu ndilo linalojulikana. Hichens (1940) amesema kuwa, mke huyu alitwa Simbe wa mwana wa Haliwewa. Inaweza kukisiwa kuwa, kutojulikana kwa majina ya hao wake wengine huenda ni kwa sababu hawakuwa wake halali. Pengine Muyaka aliwaweka rumenya tu. Sababu nyingine inaweza kuwa pengine wake hao hawakuwa maarufu tu! Kwa mfano inathibitika kuwa

wake wenza wa Mwanakupona hawakuwa maarufu kama alivyokuwa yeye. Kalima hii ina mashiko kwani mbali na kutajwa tu, hakuna chochote ambacho kimeandikwa kuhusu Mwanapepo, Mwanahamisi na Mwanakikau. Madai haya basi yanaelekeza kuiunga hoja ya Gibbe (1995: 207) kuwa, pamoja na kuwaoa wake watatu, Muyaka alikuwa ma Masuria watatu. Hali hii huenda ilisababishwa na tabia ya wanabiashara ya kusafiri kwingi ambako pia walikaa kwa muda kabla ya kurejea makwao. Katika baadhi ya mashairi yake, Muyaka amedhihirisha uwezekano wake wa kuwa na wake zaidi ya mmoja. Katika shairi hili, Muyaka anamkejeli mwanamke ambaye, kwa kutotarajia, ametembelewa na wapenzi wake watatu (Muyaka akiwa mmoja wao). Muyaka anampa mwanamke huyu mfano wa ugumu uliopo kwa mwanamke yeyote kuwa na wachumba watatu. Shairi linasema:

Mbwene mwinda na taza kuemewa
ni tomezi;
Mno vikanishangaza, hapatwa na
makuzi
Hafikiri nikiwaza, Mola ndiye
Muwawazi!
Tui na mani na mbuzi huvushwaje
dau moja
(Abdulaziz, 1979:92).

Kwa muhtasari, Muyaka anamuuliza mwanamke huyu ni wapi alipopata kuona chui, mbuzi na majani vikisafirishwa kwa pamoja katika dau moja? Chui bila shaka atataka kumla mbuzi, naye mbuzi atavamia majani kuyala! Muyaka anaonyesha kuwa mtu mwenye "bidhaa" hizi katika dau lake, hawezi kuwa na amani. Sharti mtu huyu, atakosa kufikisha bidhaa zake zote ng'ambo ya pili. Hii ndiyo hali aliyomo mwanamke anayetembelewa na wanaume watatu! Katika fumbo hili mwanamke ndiye dau, wanaume watatu wanawakilishwa na chui, mbuzi na majani, kisha safari yake ndiyo mapenzi. Bila shaka safari hiyo haiwezi kuwa ya amani.

Maelezo ya Muyaka katika shairi la 'Kimbiji Changu', pia yanaashiria uwezekano wake wa kuwa na mke zaidi ya mmoja. Katika shairi hili, Muyaka anataka kumrudia mke wake wa awali kwa vile mke huyu mwingine aliye naye amechacha kwa vitimbi. Ubeti huu unakiriri azma ya kurudia mke wake wa kitambo. Muyaka anaeleza kwamba:

Kiwinzo change kiwinzo nilipo
hikioleza
Chakuliwa matezo nami
kikinipumbaza,
Hatusa nacho ufunzo mawimbi kutoa
kweza,
Ndipo leo hakiwaza hangaama
kazekea.
(Abdulazizi, 1979:168).

Muyaka alikuwa rafiki wa viongozi wa Mombasa wa miaka ya 1814 hadi 1834. Inadaiwa kuwa Muyaka alienda ngomeni kila mara wakati wa uongozi wa Wamazrui, hususan Abdulla bin Hemed (1814-1823) na Salim bin Hemed (1824-1834), kwa mazungumzo nao (Abdullaziz, 1979: 110). Viongozi hawa wanadaiwa, walipenda mashairi ya Waswahili sana na hatima yake, wao wenyewe wakayatunga pia.

Muyaka ametunga mashairi yenye maudhui mbalimbali. Si mashairi ya siasa tu (na hii huenda inatokana na urafiki wake mkubwa na viongozi wa Mombasa waliotajwa), bali pia ametunga mashairi juu ya uhusiano wa watu, mapenzi na mambo mengine mengi yanayohusu jamii. Katika utanzu wa ushairi, imedaiwa kuwa Muyaka ameongezea amana kadhaa kama vile mtindo, umbo na msamiati kochokocho (Abdulaziz, 1979). Mwalimu sikujua katika shairi lake la wasifu, amempongeza Muyaka kwa 'kumpa taji' la mshairi Hodari. Katika shairi hilo anasema:

Nawambia pulikani, hizo zamani za
kale
Muyaka ali ni shani kwa mashairi
tuwele;
Alikingia ngomani pasiwe mkia
mbele;
Akitongoa tongole; Bwana Tela
amepata.

Mashairi ya fikira k'umbusho za
ushuhuda;
Yazingao kama dira yapao watu
faida;
Alizungukiwa na kura, Muyaka ndiye
ziyada,
Kuwezekana ni shida. Bwana Tela
amepata

(Abdulaziz, 1979: 101).

Kutokana na ushairi wa Muyaka, ni dhahiri kuwa utanzu wa ushairi umepata msingi bora ambao baadaye umeendelezwa na washairi wa karne ya ishirini kama vile marehemu Shaaban Robert, Ahmed Nasser Juma Bhalo na Abdilatif Abdallah miongoni mwa wengine (Abdulaziz, 1979).

Baada ya kutoa mchango wake katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili, inaelezwa kuwa Muyaka, aliaga dunia mwaka wa 1840. Kwa hivyo, Muyaka alifariki akiwa na miaka 64. Kwamba Muyaka alifikisha umri huu ni bayana kwa vile katika shairi 'Wole', mtunzi huyu anaonekana kusikitikia maafa yanayomkaribia katika miaka yake ya sitini. Inaonekana kuwa, alipofikisha umri huu, ugonjwa (maafa) ulianza kumwingia. Katika shairi hili Muyaka anasikitika kwa maneno:

Aliyekimbia wole, mwendo wa
myaka sitini,
Akenda umungojele, ukele mitilizini,
Ukamba ndoo tukale, mwandani,
wangu mwandani!
Akiuza unani? Ukamba: si mi woleo?
(Knappert, 1966:133)

Maradhi haya yalizidi kumnasa na baada ya kitambo cha miaka minne, Muyaka aliaga dunia. Alizikwa makaburi yanayotengewa watu wa koo za kimvita huko Mombasa karibu na kivuko cha Nyali (Abdullaziz, 1979:112). Ingawa tungo za Muyaka hazikolezi sana athari ya mitazamo na mielekeo ya dini ya Kiislamu, mtunzi huyu alikuwa mfuasi wa dhati wa dini ya Kiislamu kwani lazima awe alijifunza maandishi haya katika vyuo vya dini (Madrasa). Ili mtu yeyote yule akubaliwe kuingia chuoni, ilikuwa sharti yeye na aila yake wawe wafuasi wa dini hii. Ni muhimu kuzingatia kuwa Muyaka hakuwa shehe au kiongozi wa dini. Kwa minajili hii ilikuwa si lazima kwake kuzungumzia mambo ya kidini kindakindaki. Kwa hivyo, huenda kutodhihirika sana kwa athari ya dini hii ndio sababu inayomwelekeza mtaalamu Harries (1962) adai kuwa mtunzi huyu ametoa ushairi wa Kiswahili msikitini na kuupeleka sokoni. Huko sokoni, umaarufu wake unachachamaa kwa burudani yake safi inayotokana na tungo zinazojadili maudhui mbalimbali katika Maisha ya jamii. Vichekesho vyake na ukwasi mwingi wa lugha

na jinsi ya kuyasawiri mambo kwa hadhira yake, pia huongeza umaarufu katika kazi yake. Kama anavyosema Mwalimu Sikujua (Abdulaziz, 1979: 101):

Mashairi ya fikira k'umbusho za ushuhuda;
Yazingao kama dira yapao watu faida,
Aliangukiwa na kura, Muyaka ndiye ziyada.

Kipawa cha mtunzi huyu kinadhihirika katika jina lake! Jina 'Muyaka' katika Kiswahili cha kikale lina maana ya 'mzuri' (Gibbe, 1995: 207). Uzuri huu unafikia kilele chake katika Sanaa anayoendeleza; Sanaa ya utunzi na ulumbi wa mashairi. Kwa hivyo, si ajabu kuwa alitokea kupendwa na watu kwa ucheshi, mizaha, biashara na uhodari wake wa kutunga mashairi.

MATOKEO

Mashairi ya Muyaka

Kama nilivyokwisha kueleza awali, mashairi matano ya Muyaka yaliteuliwa ili yasaide katika kuichambua taswira ya mwanamke wa Kiswahili katika ushairi wa Kiswahili wa karne ya kumi na tisa. Mashairi haya ni: 'Kimbiji Changu', 'Siupati Usingizi', 'Nazi na Maji si Mbata', 'Utavaa nguo Gani?' na 'Kuonana na Wewe'. Nilitaja pia katika utangulizi kuwa mtunzi huandika kujihusu mwenyewe, jamii yake na wakati (kipindi) fulani katika historia. Msimamo wa utafiti huu ni kwamba mashairi ya Muyaka na hasa yale yanayoshughulikiwa, yanamhusu mwenyewe na tajriba yake katika jamii yake ya Waswahili wa karne ya kumi na tisa.

Shairi: 'Kimbiji Changu'.

Fumbo la Kimbiji/ Kidau/ Kiwinzo

Shairi la 'Kimbiji Changu' linazungumzia hali mahsusi ya Maisha ya Muyaka. Mtunzi anaelezea hali hii kwa mafumbo, kisa cha shairi kinahusu kidau na safari ya baharini. Muyaka anasimulia jinsi anavyoazimia kukirudia kidau chake cha kwanza katika kusafiria baharini. Huenda kidau anachokitumia kwa sasa kinampa matatizo. Anaeleza katika ubeti wa 1 kuwa:

Nastahabu kimbiji, kidau changu cha kwanza
Kingawa mlejileji k'welea haikupanza

Na kufa Ngozoa-Maji, yali usiku wa kiza
Ndipo leo hakiwaza haangama
Kazekea.

Muyaka, katika maelezo haya, anaonekana kama anayelinganisha vidau viwili. Uzito wa mizani unakiangukia kidau cha kwanza. Kidau hiki kinaonyeshwa kuwa na ubora fulani. Muyaka anasema, "Kingawa mlejileji k'welea haikupanza". Mshororo huu una maana kwamba, hata katika bahari yenye mawimbi makali, kidau cha kwanza hakiingizi maji yanayoweza kusababisha kuzama kwake- kidau hicho ghalibu huelea. Kidau chenye sifa hii ni cha manufaa sana kwa msafiri wa baharini. Kama ilivyoonyeshwa awali, mtunzi huyu alikuwa mwanabishara na, kwa hivyo, daima alisafirisha bidhaa akizichuuza sehemu moja hadi nyingine, kuna uwezekano kuwa nyingi ya safari zake zilikuwa za baharini. Ghalibu hakuna nahodha au abiria yeyote wa baharini asiyeona furaha anapotumia chombo chenye utulivu. Kwa sababu hii, Muyaka anaamua kukiacha kidau chake cha sasa ili akirudie kile cha zamani kwa kuwa kilimhakikishia usalama zaidi. Azma hii inajitokeza bayana katika mkarara wa shairi. Mtunzi anasema, "Ndipo leo hakiwaza haangama kazekea". Inaelekea kuwa Muyaka, alikitumia kidau chake cha kwanza kuenda kazekea ambako aliwasili salama salimini.

Katika ubeti wa 2, Muyaka anazidi kuonyesha sifa za kidau chake cha kwanza. Anadai kwamba, kila alipokiendesha kidau hiki alikifurahia kwani, safari daima ilikuwa kama mchezo unaopendeza. Anasema kuwa:

Kiwinzo changu kiwinzo nilipo
hikioleza
Chalikuwa na matezo nami
kikinipumbaza,
Hatusa nacho ufunzo mawimbi kutoa
kweza,
Ndipo leo hakiwaza haangama
kazekea.

Mtunzi anaonyesha kuwa, uzuri na urahisi wa kusafiria katika kidau chake cha kwanza ulimwezesha kupita katika sehemu ya bahari yenye mawimbi makali na hatari bila ya kushuhudia matatizo yoyote. Anaelezea juu ya safari hiyo tulivu anaposema, "Hatusa nacho

ufuzo mawimbi kutoa kweza”. Safari ya utulivu kama hiyo ni bahati na fahari kubwa kwa Muyaka. Ndipo sasa ameazimia kukirudia kidau hiki baada ya kukiacha kwa muda.

Shairi la Muyaka linaonyesha kwamba amekataa safari za hatari anazozishuhudia katika vidau vinginevyo. Sasa ameamua kukitumia kidau kimoja peke yake, nacho ni kile chake cha kwanza kabisa. Aidha, shairi hili linakusudia kutoa msimamo mpya wa Muyaka; kuwa anataka kurudia maisha yake ya hapo awali ambayo yanaonekana kuwa mazuri yanapolinganishwa na ya sasa. Maelezo ya shairi hili yanaweza kupewa ufafanuzi zaidi wa ndani kuhusu Maisha ya Muyaka. Mshairi alikusudiwa kumrudia mke wake wa kwanza. Anagundua uzuri wa mke wake wa kwanza baada ya kupata mke, (au hata wanawake) wengine, na mwisho wake kutambua kuwa mke huyo ‘hatoshi’ wala hafai! Abdulaziz (1979: 168), anadai kuwa, shairi hili linazungumzia hali ya Muyaka kumrudia mke wake baada ya kumuacha kwa muda fulani. Huenda Muyaka alimwacha mke wake kwa sababu ya kumpata mwanamke mwingine kwa muda tu! Hii ni hali ambayo wanaume wengi wanaweza kujiingiza. Hali hii pia imeonyeshwa katika shairi lingine la Muyaka: ‘Malalamiko ya mke’ (Abdulaziz, 1979). Shairi hili ni tofauti kidogo kwa sababu mhusika ni mke anayelalamika kuhusu mume wake aliyezuzuliwa na wasichana chipukizi. Sababu hii huenda pia ndiyo inayompotosha Muyaka katika shairi lake la ‘kimbiji Changu’. Lakini kama ilivyo kawaida ya Maisha, kila kukicha, mwanadamu huzidisha umri, kwani ujana ni moshi. Katika hali hii, hakuna anaye kuwa kijana milele! Kwa mujibu wa fumbo la shairi hili, ujana wa yule mwanamke anayemzuzua Muyaka unaonekana umefifia na, kwa vile jungu kuu halikosi ukoko, Muyaka anaamua kurudia mke wake wa kwanza aliye na busara na anayefahamu jinsi ya kumtunza.

Shairi hili linatoa picha mbalimbali za mwanamke. Mke wa kwanza wa Muyaka anapewa sifa mzomzo. Matumizi ya kivumishi, ‘changu’ yanathibitisha hali kuwa anayezungumziwa ni mke halali yaani mke wa ndoa ambaye ni miliki ya mume wake. Mtunzi anamwita mke huyu kimbiji, kidau na kiwinzo. Majina haya yote yana maana moja, ambayo ni dau dogo. Kidau ni chombo kidogo, chembamba, kilicho wazi na kinachotumiwa kwa kusafiri baharini. Kabla ya maajilio ya vyombo vinavyotumia mashine, vidau vilikuwa

maarufu sana kwa wavuvi wa Afrika Mashariki, Waswahili wakiwemo. Kwa hivyo, Muyaka anaulinganisha umaarufu wa mke wake wa kwanza na umaarufu wa kidau enzi hizo. Kwa kumpa sifa hii, mtunzi anaonyesha kuwa, ni vigumu kwake kujitegemea bila mke wake wa kwanza kuwepo, kama ilivyo vigumu kwa msafiri yeyote wa baharini kusafiri pasipo dau. Kwa hivyo umuhimu wa mke huyu unadhihirika.

Matumizi ya fumbo la kimbiji inazidi kuonyesha heshima anayopewa mwanamke katika jamii hii. Inyani (1994:54) anadai kuwa, jazanda hii katika jamii ya Waswahili inapotumiwa kumuashiria mwanamke huwa na maana ya mtu mwaminifu na mtiifu katika uhusiano wake na mume wake. Vile vile, jazanda hii inatumiwa kurejelea wake wanaowaheshimu mabwana zao kwa kutoshiriki uasherati. Wake wanaoashiriwa kwa jazanda hii, huwa ni wale walio na tabia njema, mapenzi yasiyotikisika na wanaojenga na kudumisha ndoa zao daima. Kwa hivyo, mke wa kwanza wa Muyaka ana sifa hizi, ambazo ndizo zinamvutia amrudie. Kwa kawaida, mume wa kupotoshwa na wanawake wa kando ya ndoa si rahisi kumrudia mke wake wa akidi. Kurudi kwake hutegemea sifa za mke huyo.

Katika shairi hili, Muyaka amesawiri picha ya mwanamke iliyo na wingi wa sifa za kutamaniwa. Kwa njia mbali mbali, mwanamke ameonyeshwa kama fundi mwenye stadi maradufu za kumjenga mume wake. Mke anakuza mapenzi, analeta furaha na anadumisha amani na utulivu katika ndoa. Hizi ni sifa za heshima. Kama anavyosema Inyani (1994:42), kwa kawaida mke ana jukumu la kufanya kazi kama ile ya dawa. Wakati wowote mume anapokuwa katika matatizo ya kimawazo, mke anahitajika kumpa suluhisho. Kwa mfano, kwa sababu ya matendo yake, yanayoonyesha mapenzi na maneno yake matamu, mume wake huliwazwa. Kwa sababu hii, inaweza kudaiwa ya kwamba kila moja ya sifa anayopewa mwanamke katika shairi la ‘kimbiji changu’, ni sifa inayomuenzi. Kwa hivyo, usawiri wa mwanamke katika shairi hili umejikita sana katika misingi ya utamaduni wa Waswahili. Nafasi hii haimfanyi mke kuwa chombo, (kidau) kama anavyodai Imbosa (1990). La hashi! mke analinganishwa na kidau kijazanda kwa sababu ya kuonyesha umuhimu wa nafasi yake katika maisha ya mume wake katika ndoa yao. Katika muktadha wa

kusafiri baharini, kati ya msafiri na dau hakuna aliye bora kuliko mwingine. Ili safari itengenee, ni sharti msafiri na dau viwepo. Upande mmoja kati ya hizi mbili usipokuwapo safari haiwi. Ni vivyo hivyo katika ndoa. Kati ya mke na mume hakuna mwenye faida kuzidi mwenziwe, kwani mmoja wao asipokuwapo basi ndoa kati yao haiyumkini tena. Hii ndio hali inayodhihirika katika uchambuzi huu.

Fumbo la Kazekea

Inavyotambulika kuwa kidau chake cha kwanza ndicho chenye utulivu, vivyo hivyo ndivyo inavyobainika kuwa mke huyo wa kwanza ndiye mwenye kumletea raha, utulivu na amani katika Maisha. Sifa ya utulivu kwa mke huyu inajitokeza katika mkarara wa shairi hili, Muyaka anapotaja mahali paitwapo Kazekea. Imeelezwa, hapo awali, kuwa Kazekea ni mahali palipojulikana kwa utulivu wa bahari. Mtunzi anaposema kuwa kidau chake kinampeleka huko anaonyesha kuwa ni mke wa kwanza anayejua jinsi ya kumpa utulivu. Ni wazi kwamba, iwapo mke anafahamu namna ya kumletea mume wake utulivu, basi yeye binafsi ana sifa hiyo ya utulivu. Aidha sifa ya mke wa kwanza kuwa na bashasha na vicheko vya kumfurahisha mume wake inadhihirika katika maelezo kuwa, “Chalikuwa na mateso nami kikinipumbaza”. Katika ndoa ni sharti bwana na bibi wawe na maelewano mazuri ambayo yatawafanya kuaminiana, kuelewana na kufarijiana. Mambo haya humpa kila mmoja imani kwa mwenzake na hivyo basi kuongeza dhati ya uhusiano wao. Ndoa hii ya maelewano, kamwe haikosi furaha, vicheko na mizaha ya kimapenzi baina ya mke na mume wake. Hili limezungumziwa bayana katika Utenzi wa Mwanakupona (Wandera 1996). Utamaduni wa Waswahili umezingatia sana ndoa ya aina hii. Mathalan, mwanamke wa Kiswahili ameelekezwa ajitokeze bayana katika kufanikisha ndoa ya maelewano. Kwa hivyo, Muyaka katika maelezo yake, anadhihirisha kwamba mke wake wa kwanza anajua jukumu hili na analitekeleza barabara. mke huyu ni ishara ya utulivu, huruma, ukarimu pamoja na mapenzi yanayojaa pumbazi. Inaonekana kuwa, Muyaka sasa amegundua kwamba, “Usiache mbachao kwa mswala upitao”.

Matumizi ya fumbo la kimbiji inazidi kuonyesha heshima anayopewa mwanamke katika jamii hii. Inyani (1994:54) anadai kuwa, jazanda hii katika jamii ya Waswahili inapotumiwa kumuashiria mwanamke huwa

na maana ya mtu mwaminifu na mtiifu katika uhusiano wake na mume wake. Vile vile, jazanda hii inatumiwa kurejelea wake wanaowaheshimu mabwana zao kwa kutoshiriki uasherati. Wake wanaoashiriwa kwa jazanda hii, huwa ni wale walio na tabia njema, mapenzi yasiyotikisika na wanaojenga na kudumisha ndoa zao daima. Kwa hivyo, mke wa kwanza wa Muyaka ana sifa hizi, ambazo ndizo zinamvutia amrudie. Kwa kawaida, mume wa kupotoshwa na wanawake wa kando ya ndoa si rahisi kumrudia mke wake wa akidi. Kurudi kwake hutegemea sifa za mke huyo.

Katika shairi hili, Muyaka amesawiri picha ya mwanamke iliyo na wingi wa sifa za kutamaniwa. Kwa njia mbali mbali, mwanamke ameonyeshwa kama fundi mwenye stadi maradufu za kumjenga mume wake. Mke anakuza mapenzi, analeta furaha na anadumisha amani na utulivu katika ndoa. Hizi ni sifa za heshima. Kama anavyosema Inyani (1994:42), kwa kawaida mke ana jukumu la kufanya kazi kama ile ya dawa. Wakati wowote mume anapokuwa katika matatizo ya kimawazo, mke anahitajika kumpa suluhisho. Kwa mfano, kwa sababu ya matendo yake, yanayoonyesha mapenzi na maneno yake matamu, mume wake huliwazwa. Kwa sababu hii, inaweza kudaiwa ya kwamba kila moja ya sifa anayopewa mwanamke katika shairi la ‘kimbiji changu’, ni sifa inayomuenzi. Kwa hivyo, usawiri wa mwanamke katika shairi hili umejikita sana katika misingi ya utamaduni wa Waswahili. Nafasi hii haimfanyi mke kuwa chombo, (kidau) kama anavyodai Imbosa (1990). La hash! mke analinganishwa na kidau kijazanda kwa sababu ya kuonyesha umuhimu wa nafasi yake katika maisha ya mume wake katika ndoa yao. Katika muktadha wa kusafiri baharini, kati ya msafiri na dau hakuna aliye bora kuliko mwingine. Ili safari itengenee, ni sharti msafiri na dau viwepo. Upande mmoja kati ya hizi mbili usipokuwapo safari haiwi. Ni vivyo hivyo katika ndoa. Kati ya mke na mume hakuna mwenye faida kuzidi mwenziwe, kwani mmoja wao asipokuwapo basi ndoa kati yao haiyumkini tena. Hii ndio hali inayodhihirika katika uchambuzi huu.

Matumizi ya fumbo la kimbiji inazidi kuonyesha heshima anayopewa mwanamke katika jamii hii. Inyani (1994:54) anadai kuwa, jazanda hii katika jamii ya Waswahili inapotumiwa kumuashiria mwanamke huwa na maana ya mtu mwaminifu na mtiifu katika uhusiano

wake na mume wake. Vile vile, jazanda hii inatumiwa kurejelea wake wanaowaheshimu mabwana zao kwa kutoshiriki uasherati. Wake wanaoashiriwa kwa jazanda hii, huwa ni wale walio na tabia njema, mapenzi yasiyotikisika na wanaojenga na kudumisha ndoa zao daima. Kwa hivyo, mke wa kwanza wa Muyaka ana sifa hizi, ambazo ndizo zinamvutia amrudie. Kwa kawaida, mume wa kupotoshwa na wanawake wa kando ya ndoa si rahisi kumrudia mke wake wa akidi. Kurudi kwake hutegemea sifa za mke huyo.

Katika shairi hili, Muyaka amesawiri picha ya mwanamke iliyo na wingi wa sifa za kutamaniwa. Kwa njia mbali mbali, mwanamke ameonyeshwa kama fundi mwenye stadi maradufu za kumjenga mume wake. Mke anakuza mapenzi, analeta furaha na anadumisha amani na utulivu katika ndoa. Hizi ni sifa za heshima. Kama anavyosema Inyani (1994:42), kwa kawaida mke ana jukumu la kufanya kazi kama ile ya dawa. Wakati wowote mume anapokuwa katika matatizo ya kimawazo, mke anahitajika kumpa suluhisho. Kwa mfano, kwa sababu ya matendo yake, yanayoonyesha mapenzi na maneno yake matamu, mume wake huliwazwa. Kwa sababu hii, inaweza kudaiwa ya kwamba kila moja ya sifa anayopewa mwanamke katika shairi la 'kimbiji changu', ni sifa inayomuenzi. Kwa hivyo, usawiri wa mwanamke katika shairi hili umejikita sana katika misingi ya utamaduni wa Waswahili. Nafasi hii haimfanyi mke kuwa chombo, (kidau) kama anavyodai Imbosa (1990). La hasha! mke analinganishwa na kidau kijazanda kwa sababu ya kuonyesha umuhimu wa nafasi yake katika maisha ya mume wake katika ndoa yao. Katika muktadha wa kusafiri baharini, kati ya msafiri na dau hakuna aliye bora kuliko mwingine. Ili safari itengenee, ni sharti msafiri na dau viwepo. Upande mmoja kati ya hizi mbili usipokuwapo safari haiwi. Ni vivyo hivyo katika ndoa. Kati ya mke na mume hakuna mwenye faida kuzidi mwenziwe, kwani mmoja wao asipokuwapo basi ndoa kati yao haiyumkini tena. Hii ndio hali inayodhihirika katika uchambuzi huu.

Matumizi ya fumbo la kimbiji inazidi kuonyesha heshima anayopewa mwanamke katika jamii hii. Inyani (1994:54) anadai kuwa, jazanda hii katika jamii ya Waswahili inapotumiwa kumuashiria mwanamke huwa na maana ya mtu mwaminifu na mtiifu katika uhusiano wake na mume wake. Vile vile, jazanda hii inatumiwa

kurejelea wake wanaowaheshimu mabwana zao kwa kutoshiriki uasherati. Wake wanaoashiriwa kwa jazanda hii, huwa ni wale walio na tabia njema, mapenzi yasiyotikisika na wanaojenga na kudumisha ndoa zao daima. Kwa hivyo, mke wa kwanza wa Muyaka ana sifa hizi, ambazo ndizo zinamvutia amrudie. Kwa kawaida, mume wa kupotoshwa na wanawake wa kando ya ndoa si rahisi kumrudia mke wake wa akidi. Kurudi kwake hutegemea sifa za mke huyo.

Katika shairi hili, Muyaka amesawiri picha ya mwanamke iliyo na wingi wa sifa za kutamaniwa. Kwa njia mbali mbali, mwanamke ameonyeshwa kama fundi mwenye stadi maradufu za kumjenga mume wake. Mke anakuza mapenzi, analeta furaha na anadumisha amani na utulivu katika ndoa. Hizi ni sifa za heshima. Kama anavyosema Inyani (1994:42), kwa kawaida mke ana jukumu la kufanya kazi kama ile ya dawa. Wakati wowote mume anapokuwa katika matatizo ya kimawazo, mke anahitajika kumpa suluhisho. Kwa mfano, kwa sababu ya matendo yake, yanayoonyesha mapenzi na maneno yake matamu, mume wake huliwazwa. Kwa sababu hii, inaweza kudaiwa ya kwamba kila moja ya sifa anayopewa mwanamke katika shairi la 'kimbiji changu', ni sifa inayomuenzi. Kwa hivyo, usawiri wa mwanamke katika shairi hili umejikita sana katika misingi ya utamaduni wa Waswahili. Nafasi hii haimfanyi mke kuwa chombo, (kidau) kama anavyodai Imbosa (1990). La hasha! mke analinganishwa na kidau kijazanda kwa sababu ya kuonyesha umuhimu wa nafasi yake katika maisha ya mume wake katika ndoa yao. Katika muktadha wa kusafiri baharini, kati ya msafiri na dau hakuna aliye bora kuliko mwingine. Ili safari itengenee, ni sharti msafiri na dau viwepo. Upande mmoja kati ya hizi mbili usipokuwapo safari haiwi. Ni vivyo hivyo katika ndoa. Kati ya mke na mume hakuna mwenye faida kuzidi mwenziwe, kwani mmoja wao asipokuwapo basi ndoa kati yao haiyumkini tena. Hii ndio hali inayodhihirika katika uchambuzi huu.

Matumizi ya fumbo la kimbiji inazidi kuonyesha heshima anayopewa mwanamke katika jamii hii. Inyani (1994:54) anadai kuwa, jazanda hii katika jamii ya Waswahili inapotumiwa kumuashiria mwanamke huwa na maana ya mtu mwaminifu na mtiifu katika uhusiano wake na mume wake. Vile vile, jazanda hii inatumiwa

kutoshiriki uasherati. Wake wanaoashiriwa kwa jazanda hii, huwa ni wale walio na tabia njema, mapenzi yasiyotikisika na wanaojenga na kudumisha ndoa zao daima. Kwa hivyo, mke wa kwanza wa Muyaka ana sifa hizi, ambazo ndizo zinamvutia amrudie. Kwa kawaida, mume wa kupotoshwa na wanawake wa kando ya ndoa si rahisi kumrudia mke wake wa akidi. Kurudi kwake hutegemea sifa za mke huyo.

Katika shairi hili, Muyaka amesawiri picha ya mwanamke iliyo na wingi wa sifa za kutamaniwa. Kwa njia mbali mbali, mwanamke ameonyeshwa kama fundi mwenye stadi maradufu za kumjenga mume wake. Mke anakuzi mapenzi, analeta furaha na anadumisha amani na utulivu katika ndoa. Hizi ni sifa za heshima. Kama anavyosema Inyani (1994:42), kwa kawaida mke ana jukumu la kufanya kazi kama ile ya dawa. Wakati wowote mume anapokuwa katika matatizo ya kimawazo, mke anahitajika kumpa suluhisho. Kwa mfano, kwa sababu ya matendo yake, yanayoonyesha mapenzi na maneno yake matamu, mume wake huliwazwa. Kwa sababu hii, inaweza kudaiwa ya kwamba kila moja ya sifa anayopewa mwanamke katika shairi la 'kimbiji changu', ni sifa inayomuuzi.

Kwa hivyo, usawiri wa mwanamke katika shairi hili umejikita sana katika misingi ya utamaduni wa Waswahili. Nafasi hii haimfanyi mke kuwa chombo, (kidau) kama anavyodai Imbosa (1990). La hasha! mke analinganishwa na kidau kijazanda kwa sababu ya kuonyesha umuhimu wa nafasi yake katika maisha ya mume wake katika ndoa yao. Katika muktadha wa kusafiri baharini, kati ya msafiri na dau hakuna aliye bora kuliko mwingine. Ili safari itengenee, ni sharti msafiri na dau viwepo. Upande mmoja kati ya hizi mbili usipokuwapo safari haiwi. Ni vivyo hivyo katika ndoa. Kati ya mke na mume hakuna mwenye faida kuzidi mwenziwe, kwani mmoja wao asipokuwapo basi ndoa kati yao haiyumkini tena. Hii ndio hali inayodhihirika katika uchambuzi huu.

Fumbo la Kiambishi 'Ki'

Kutokana na maelezo ya fumbo la shairi hili, Muyaka amemjazia mke wake wa kwanza sifa nzuri zenye haiba kubwa. Kwa kumuita kimbiji, kiwinzo na kidau, mtunzi anaonyesha jinsi alivyo na mapenzi ya dhati kwake. Kwa mujibu wa maelezo ya inyani (1994:53)

matumizi ya kiambishi "ki" katika Kiswahili huashiria urembo. Kwa mwelekeo huu, Muyaka anamuona mke wake kuwa mrembo. Imbosa (1990) anasema kuwa, kiambishi "ki" kinapotumiwa kama neno la sifa, huashiria udogo na pia mapenzi fulani kwa kile kinachozungumziwa. Kwa hivyo, picha inavyojitokeza kwa maelezo ya shairi hili, hasa inapomrejelea mwanamke, ni ile ya mtu mrembo na anayependwa.

Shairi: Siupati Usingizi Fumbo la Njiwa

Shairi hili ni la mapenzi. Muyaka anaonyesha jinsi mapenzi yake kwa mwanamke fulani yanamwingiza katika lindi la mawazo kiasi kwamba hapati usingizi wowote. Mpenzi wake ako mbali naye na ndio sababu analazimika kumtuma mjumbe apeleke lisala kwake. Muyaka anazungumzia haya katika ubeti wa kwanza, anaposema:

Risala wangu basiri, leo napenda
kutuma
Enenda ndiwa huuri, mwenyi cheo na
hishima:
Fika ukamhubiri haya t'akayokutuma
Namuapia Karima, siupati usingizi

Mtunzi anamwagiza tarishi wake anayemsifu kuwa mwelezi na hodari kwamba aupeleke ujumbe huo maarufu kwa mwanamke fulani, mwenye uzuri wa kupindukia na macho maangavu kama njiwa. Mwanamke huyo pia ana cheo na heshima katika jamii. Fumbo la Njiwa huuri inaonyesha jinsi mtunzi anayomwelewa mpenzi wake. Uzuri wa mpenzi huyu unalinganishwa na uzuri wa njiwa. Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu njiwa ni 'ndege mkubwa kuliko tetere na ambaye hufugwa'. Kwa maana hii, Muyaka huenda anadokeza kwamba huyo ndiye mwanamke ambaye amemchagua kuwa mke wake siku za usoni.

Inakisiwa hivi, kwa sababu, kama anavyoelezea Wandera (1996) wanawake Waswahili kwa kawaida hukaa nyumbani na huko ndiko wanakoendeshea shughuli zao za kila siku. Huku kukaa kwao nyumbani kwaweza kumithilishwa na kufugwa kwa njiwa-wa kukaa nyumbani. Aidha, kwa mujibu wa sifa za njiwa wanapokuwa nyumbani kwamba huvutia kwa rangi nzuri na sauti nyororo wanapocheza. Mtunzi pia anaonyesha haja yake ya kumpata mwanamke wa aina

hiyo ili amfurahishe na kumchangamsha pale nyumbani. Ni wazi kwamba, mtu yeyote anapokuwa peke yake hukumbwa na upweke. Muyaka hataki kuwa katika hali ya ukiwa na ndio sababu anamtaka mpenzi wake awe pale nyumbani. Kwa hivyo, si kioja Muyaka kumwambia mjumbe wake aende amhubirie mpenzi wake. Matumizi ya neno 'hubiri' yanatumika pia kuthibitisha haja kubwa ya dharura aliyonayo Muyaka juu ya kumpata mwanamke huyu.

Fumbo la Cheo na Heshima

Muyaka pia, ameongezea sifa nyingine katika kumwelezea mpenzi wake kama inavyodhihirika katika ubeti wa 1. Pamwe na kumlinganisha na njiwa huuri kama ilivyoonyeshwa hapo juu amemwita "Mwenye cheo na heshima". Katika jamii ya Waswahili wa karne ya kumi na tisa, utabaka ulishamiri sana. Watu walijitambulisha kwa nasaba zao. Wale waliozaliwa katika familia za utukufu na mali na uongozi walipewa heshima sana. Kujihusisha na watu wa tabaka la juu au kuwa mmoja wao, kulimpa mtu cheo na heshima katika jamii hii. Kwa vile tabaka hili lilijiweza kwa hali na mali, wanawake wao aghalabu ndio walioweza kulelewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na utamaduni wa Waswahili kwa kila namna. Hali hii iliwapa wanawake wa tabaka hili nafasi bora ya kutekelea wajibu wao sawasawa katika ndoa zao. Mwanamke anayetumiwa risala katika shairi hili, ni mmoja wa wanawake wa tabaka la juu. Kwa sababu hii ni sharti apewe haki yake kwa kuheshimiwa na kusifiwa inavyostahilika katika jamii hii.

Maelezo ya ubeti wa 2 yanaendeleza sifa za mwanamke huyu. Muyaka anazidi kuonyesha jinsi mwanamke huyu anavyostahili heshima kwa namna anavyomwagiza taarishi kutenda pindi afikapo kwake. Muyaka anashauri hivi katika ubeti wa 2:

Wisapo mpa salamu, ndiwa asio
mfano
Mwema wa kutakalamu fasiha
yakwe maneno
Ni mwema wa tabasamu, na
mchache wa matukano
Hasa himuwaza mno, siupati usingizi,

Ubeti huu unaelezea kuwa uzuri wa mwanamke huyu hauwezi kufananishwa na chochote. Hii ni kwa vile mwanamke huyu ni mrembo na mzuri kuliko chochote

kile. Maadamu mwanamke huyu amepewa sifa hii ya uzuri, mtunzi anaongezea kwamba maneno yake ni ya ufasaha na hatumii matusi na haropokwi ovyo ovyo. Muyaka anaujumlisha uzuri huu wote, kwa kuupatia sifa ya tabasamu za mrembo huyu, ambazo anadai, humkosesha usingizi kila anapomwazia. Sifa hizi anazozielezea Muyaka zinatoa picha ya mwanamke anayevutia. Picha hii ni ya kiumbe mrembo, mcheshi, mwema, asiyeropokwa ovyo ovyo na anayesema kwa ufasaha, Chambilecho Waswahili, "Kauli yako mizani". Ubeti wa mwisho wa shairi hili, sawa na ule wa pili hauishi kufululiza sifa za huyu mwanamke anayechumbiwa na Muyaka. Sifa hizi ndizo zinamsukuma Muyaka kumfahamisha mjumbe jinsi atakavyofanya atakapomkaribia mwanamke huyu. Muyaka anasema:

Wisapo mkurubia, ndiwa mwema wa
mangani:
Enda kwa kunyenyekea upomoke
maguuni,
Kisa umweleze pia yangu yaliyo
moyoni,
Mato yangu hayaoni kwa kukosa
usingizi

Katika ubeti huu Muyaka anaainisha njiwa anayemzungumzia. Katika ubeti wa 1 amemtaja kuwa ni njiwa huuri. Anafafanua zaidi kuwa njiwa huyu ni wa mangani yaani njiwa wa kufugwa. Mtunzi kwa hivyo, anadokeza kuwa kuna aina mbili ya njiwa: yule wa kufugwa na yule wa mwingi. Muyaka anapozungumzia njiwa, anarejelea yule wa mangani ambaye kwa kawaida huwa na uzuri mwingi zaidi anapolinganishwa na ule wa mwingi. Kwa mwelekeo huu, uzuri wa binti huyu anayepelekewa risala, ni ule unaoweza kumithilishwa na uzuri wa njiwa wa kufugwa peke yake. Pia, mwanamke huyu analinganishwa na njiwa wa mangani kwa jinsi alivyo bibi wa kushinda nyumbani, kama ilivyo desturi ya wanawake wa Kiswahili hususan, wa tabaka la juu. Hii ndio sababu mjumbe anashauriwa aende kwa unyenyekevu na pia amuangukie mwanamke huyu miguuni! Katika jamii ya Waswahili, kitendo cha kumwangukia mtu miguuni au kumuosha miguu baada ya safari, ni heshima isiyoyana na kifani (Saagaf, mhojiwa). Muyaka anaposhauri tarishi anyenyekee na kumwangukia mpenzi wake miguuni, anatoa heshima zake zote kwake. Aidha, hiki ni kitendo kinachoweza

kumithilishwa na kile cha kuabudu. Inaweza kudaiwa kuwa, Muyaka ‘anamwabudu’ mwanamke huyu. Abdulaziz (1979:201) anakisia kuwa, huenda Muyaka anatuma risala hii ili kuomba msamaha kwa jambo fulani alilomtendea mpenzi wake. Huu ndio ukweli unaojitokeza anapoelezea kuwa ‘mato yangu hayaoni kwa kukosa usingizi’. Kwa hakika Muyaka hawezi kuingiwa ‘upofu’ iwapo anayeusababisha hana manufaa makubwa kwake!

Shairi: Nazi na Maji si Mbata Fumbo la Nazi

Katika shairi hili, Muyaka anazungumzia mwanamke fulani ambaye ni mrembo wa kupindukia lakini amepungukiwa na uwezo fulani. Mwandishi anauelezea upungufu huu kwa fumbo katika kibwagizo cha shairi hili. Huenda kisa na maana ya kutumia fumbo, ni kusitiri ‘ukali’ wa ujumbe anaomwambia mwanamke huyu. Fumbo hili amelitunga kwa kutumia mfano wa tunda linaoleleweka licha ya kutumiwa na takriban kila mmoja katika jamii husika. Hili ni tunda la nazi. Muyaka anauelezea sifa za urembo wa mwanamke huyu katika ubeti wa 1 kwa maneno yafuatayo:

Mmbeja, mke wa shani, wenzio
ulowapita
Uzuri wako wasini, hakuna wa
kuupata
Akuweneo launi, k’wamba upekwe
mafuta!
Nazi na maji si mbata kutoa mea i
nani?

Muyaka anaanza kwa kumsifu mwanamke kuwa urembo wake ni wa ajabu na kwamba hakuna mwanamke mwingine anayeweza kulinganishwa naye. Kulingana na mwandishi, urembo huu upo katika kibwagizo, uzuri huu upo katika sura, umbo na ngozi laini na nyororo. Lakini, mtunzi anamuuliza katika kibwagizo, uzuri huu una faida gani iwapo hauzai matunda? Fumbo hili lina ujumbe kwamba ijapokuwa mwanamke huyu ana uzuri na urembo maradufu, hawezi kupata mtoto! Muyaka anaonyesha jambo hili kwa kutumia Jazanda. Analinganisha urembo wa mwanamke huyu na nazi yenye maji, hali kadhalika utasa wake anaulinganisha na nazi kavu (mbata). Katika kiitikio cha shairi hili, anauliza ni aina ipi ya nazi inayoweza kua na kuwa mnazi ili iweze kuzaa matunda

ya nazi tena? Aidha, anachomaanisha Muyaka katika maelezo yake hapa ni kuwa, urembo wa mwanamke huyu, fauka ya kutokuwa na kifani, hauna manufaa kwani hata akiolewa hawezi kuzaa watoto. Jamii ya Waswahili huthamini sana watoto ambao huwa kilele cha ndoa zao (Wandera, 1996). Kwa mwelekeo huu, ndoa isiyokuwa na watoto haiwezi kutajika kuwa imefaulu! Inyani (1994:30) anadai kuwa, ndoa isiyokuwa na watoto katika jamii ya Waswahili, haiheshimiwi bali inahurumiwa na hata kudharauliwa. Kukosa mtoto ni mojawapo ya sababu zinazohalalisha taasisi ya ukewenza katika jamii ya Waswahili. Ndoa kama hii, aghalabu huwa haina furaha. Mume mara nyingi hulazimika kumwoa mke mwingine akiwa na matumaini ya kuwapata watoto. Ajabu ni kuwa mke huyo tasa, ndiye anayempa mume wake idhini ya kuoa mke mwingine, la sivyo, mume huyo hawezi kuoa mke mwingine (Sheikh Nabhany-Mhojiwa).

Hali ya mke kutoweza kupata mtoto inaweza kuishia katika talaka. Hii ni kwa sababu, aghalabu mwanamke tasa hutafuta njia zote zile zitakazomwezesha kupata angalau mtoto. Katika hali hii, ya kuchanganyikiwa, mke huyu anaweza kuzini akiwa na matumaini kuwa huenda kitendo hicho kitaweza kumwondolea fedheha ya kuwa tasa, miongoni mwa wenzake. Uzinifu ni dhambi kubwa, hasa katika jamii inayoshikilia mafunzo ya dini ya Kiislamu. Adhabu yake kawaida huwa ni kuuawa kwa mijeledi katika Kurani, sura ya 24 aya ya 2. Adhabu kamili ya mwanamke na mwanamume wanaozini imeainishwa hivi:

Mzinifu mwanamke na mzinifu
mwanamume,
Mpigeni kila mmoja katika wao
mijeledi (bakora)
Mia, wala isiwashikeni kwa ajili yao
huruma
Katika (kupitisha) hukumu hii ya
Mwenyezi
Mungu na siku ya Mwisho. Na
lishuhudi
adhabu yao (hii) kundi la Waislamu.

Hata hivyo, ni sharti kitendo hicho kiwe kimeshuhudiwa na watu watatu. Kwa mwelekeo huu, si rahisi kumuua mzinifu kwa kuwa, si rahisi kuwapata watu watatu wamekusanyika kwa pamoja, ili kuweza kushuhudia kitendo hiki ambacho kwa kawaida

hufanywa kwa siri. Hata hivyo, panapo moshi pana moto, mume wa tasa huyo lazima atapata fununu kuhusu tabia ya mke wake. Ingawa hakuna shahidi mahsusi, hali hii inaweza kuleta uhasama mkali ndani ya nyumba. Uhasama ukizidi nyumbani bila ya kusameheana, talaka inaweza kutolewa. Hali ya mke kutoweza kupata watoto, licha ya kuwa tatizo la kimaumbile, kwa kiasi kikubwa si jambo linalokubaliwa katika jamii ya nyingi za Kiafrika (Wandera-Simwa, 2015). Mwanamke anayekuwa katika hali hii, aghalabu, huonekana kana kwamba hajakamilika. Hii ndio hali anayoashiria Muyaka anapomwelezea mwanamke huyu ukweli wa hali hiyo yake ya kusikitisha.

Maelezo ya ubeti wa 2 yanaonyesha nia ya Muyaka ya kumtanabahisha mwanamke huyo juu ya hali yake. Kulingana na jinsi mtunzi anavyomsaili mwanamke huyo, kuna uwezekano kuwa, mwanamke huyo ana maringo mengi, ambayo huenda aliyaelekeza kwa Muyaka wakati fulani. Kwa hivyo, Muyaka anaonekana kuwa anamzindua almuradi apunguze madaha kwa watu. Muyaka anafanya hivyo kwa sababu, anafahamu kuwa, mwanamke ambaye hawezi kupata watoto katika jamii yake hapewi heshima mithili ya yule mwenye watoto. Huenda Muyaka anatumia matarajio ya jamii yake kumhusu mwanamke katika ndoa ili amshambulie mwanamke ambaye pengine amekataa kushiriki mapenzi naye. Muyaka anaonyesha ukakamavu anapozungumzia hali hiyo, ambayo kwa kawaida haitajwi hadharani, hasa ikiwa mhusika mwenyewe yupo!] Inakisiwa kuwa, ukakamavu huu ameupata kutokana na kinyongo ambacho amekishikilia, kwa sababu ya kukataliwa na mwanamke huyo. Anamuuliza:

N'ambia, nipate jua, siangae ukasita,
Usililie ukiwa kwa ambae ni mkata,
Mwenye kuuza k'wambiwa, nambia
limenipata;
Nazi na maji si mata, kutoa mea i
nani?

Ubeti huu unaelezea kuwa Muyaka anamkabili mwanamke huyo ana kwa ana na kumuuliza juu ya hali yake. Muyaka anatarajia mwanamke huyo ampe jibu bila kusita. Anamuasa asisingizie upweke namna wanavyofanya maskini, kusudi waonewe huruma, kwa sababu yeye si maskini. Bila shaka, maskini hawezi kujikwatua anavyojipamba mwanamke huyo.

Kujirembesha kwake kunamfanya asiweze kulinganishwa na yeyote, kwa urembo! Ujasiri huu wa kumkabili mwanamke huyo jinsi hii, ndio unaoelekeza kudai kwamba, mtunzi ana nia mahsusi, ya kutaka kumjulisha mwanamke kuwa ana upungufu fulani wa kimaumbile! Mtunzi anatumia mbinu ya kinaya kumsihi mwanamke huyo ajibu swali lake. Kinaya cha Muyaka kinadhihirika katika maneno yake; “mwenye kuuza k'wambia, nambia limenipata;” Ana maana kuwa, kila mwenye kuuliza swali juu ya jambo fulani, hutarajia majibu kwani huwa hafahamu jambo hilo. Madai ya Muyaka katika maelezo haya si ya kweli. Yeye anajua sawasawa kwamba, nazi yam aji ndiyo inayomea na wala sio mbata. Kwa vile azma yake ni kumtia mwanamke huyo uchungu, anataka mwenyewe ajibu swali hili. Muyaka anaonekana kukiuka mipaka ya utu anapotumia mbinu hii. Kwa kawaida, mtu mwenye upungufu fulani wa kimaumbile huwa anaonewa imani na kuhurumuwa. Maelezo ya Muyaka yanaenda kinyume na hali hii. Yeye anaonekana anamsuta mwanamke huyo. Kutokana na kitendo hiki cha mtunzi, ndipo inasisitizwa kuwa Muyaka ana sababu zake za kibinafsi zinazomsukuma katika kumkashifu mwanamke huyo. Kama ilivyoelezwa awali, huenda Muyaka ametumia ‘ukali’ huu kwa sababu mwanamke huyo alimkataa wakati fulani. Aidha, ni bayana kwamba kwa sifa zake za urembo usio na kifani, mwanamke huyo ametamaniwa na wanaume wengi Muyaka akiwa mmoja wao. Muyaka, anapokataliwa, anaamua kumshambulia. Ilivyoonyeshwa hapo awali, Muyaka hakuwa na sifa nzuri miongoni mwa baadhi ya wanawake wa Mombasa (Abdulaziz 1979). Ili kulipiza kisasi hicho cha kudharauliwa na wanawake hao, Muyaka anatumia fursa yoyote ile itakayomwezesha kuonekana mshindi katika vita vyake vya baridi dhidi ya wanawake hao.

Picha ya mwanamke anayojenga Muyaka katika shairi la “Nazi na maji si mbata” inaweza kueleweka katika njia mbili. Katika njia ya kwanza, ni muhimu kubainisha kuwa kitendo cha mtunzi kwa mwanamke huyo kimetokana na tajriba yake ya kimaisha. Wengi wa wanawake walimkejeli kwa sababu ya ukosefu wake wa fedha, hali ambayo ilimfanya asiweze kuyamudu maisha yake ilivyotarajiwa kwa mtu wa wastani katika jamii hii (Abdulaziz 1979). Kutokana na kudharauliwa huku, Muyaka ametunga mashairi ambayo yanawabeza wanawake hao. Kwa hivyo, picha hii ya mwanamke inayojitokeza haiwezi kuchukuliwa kuwa

ya mkataa kuhusu mwanamke katika jamii ya Waswahili! Kwa kiasi kikubwa, picha hii inahitaji kuangaliwa kama ya kibinafsi. Hii ni picha inayotolewa na mtu mwenye 'hasira' juu ya wanawake. Kwa hivyo, si ajabu kwamba Muyaka anajaribu kuonyesha kuwa mwanamke asiyezaa ni mtu asiye na faida yeyote katika jamii.

Katika hali hii ya 'hasira', hali ya kulipiza kisasi kwa kudharauliwa na wanawake, Muyaka pia ameweza kutoa picha nyingine ya kumuenzi mwanamke. Picha hii ni ya mwanamke nadhifu na mwenye umbo la kuvutia. Kama inavyojitokeleza katika *Utenzi wa Mwanakupona*, mwanamke wa Kiswahili hufunzwa juu ya usafi wa mwili wake, wa nyumba na mazingira yake. Kwa hakika, urembo wa wanawake Waswahili si wa uzuri wa sura pekee, bali pia mwanamke hutarajiwa kujipaka hina mikononi na miguuni na kwa wanaojimudu kwa mali, kuongezea vitu vya dhahabu, shanga, vidani na hata hirizi zinazoaminiwa kwamba, huleta dua njema kwa mwenye kuzivaa. Urembo wa mapambo kwa mwanamke katika shairi hili umeelezwa. Mwanamke anayezungumziwa amejaza mapambo ya kila aina, na si ajabu kuwa hakuna mwanamke mwingine wa kumzidi. Muyaka kwa kutumia huu mfano, ameweza kuonyesha sifa halisi za mwanamke katika jamii ya wakati wake. Hii ndiyo picha halisi ya mwanamke anayethaminiwa katika jamii ya wakati wake. Ndiyo picha halisi ya mwanamke anayethaminiwa katika jamii ya Waswahili ya kipindi cha historia cha wakati huo. Itakumbukwa kuwa, ni katika kipindi hicho ambapo mapambo kwa wanawake yalizingatiwa sana kwa vile, mke alikuwa wa kufanyiwa kazi za sulubu na mume wake, ilihali yeye akibaki pale nyumbani kufanya kazi ndogo ndogo tu. Hali hii ilimpa wakati wa kutosha kushughulikia mapambo yake na usafi wa mwili wake na wa nyumba yake. Njia moja ya kudhihirisha urembo wake ilikuwa mapambo yake (Wandera, 1996). Katika shairi hili, inadhihirika kuwa, licha ya Muyaka kumshambulia mwanamke kwa sababu huenda alikataa kuwa mpenzi wake, ameweza pia kuchora picha ya mwanamke anayesifika katika jamii yake. Picha hii inaonyesha matarajio ya jamii hii, kumhusu mke katika ndoa.

Shairi: Utavaa nguo Gani?

Fumbo la nguo

Katika shairi hili, Muyaka amesawiri picha ya jinsi maisha ya ndoa yalivyo panapotokea switafahamu

baina ya mke na mume. Kisa cha shairi hili, kinazungumzia mume anayemkejeli mke wake kwa sababu ya utovu wake wa nidhamu. Pamoja na kutomnunulia nguo mpya ya kuvaa, mume huyu pia, anamnyima mke wake ruhusa ya kwenda katika sherehe. Mwanamke anabidiika kukaa nyumbani. Hana njia yoyote ya kutoka kwa vile, mume wake kama mchungwa wake, na kiongozi wa nyumba yao, ameamua kuwa abaki pale nyumbani. Hali hii inajitokeza sana katika jamii ya Waswahili. Mume anapomnyima mke wake ruhusa ya kutoka, huwa ana sababu zake maalum za kufanya hivyo. Inyani (1994: 38) anaelezea kuwa, mume anayepata mke mzuri, kwa tabia na urembo, kwa kawaida hamkubalii mtu yeyote apate nafasi ya kumshawishi dhidi yake. Mume katika hali hii, huwa tayari kumzuia mke wake kwa hali zote zile, hata ikiwa itahitajika kumfungia nyumbani ili asiweze kutangamana na watu wa aina hiyo. Muyaka huenda anakisia kuwa hali hii inaweza kutokea katika sherehe. Hii huenda ndio mojawapo ya sababu zinazomfanya amkataze mke wake kuenda kwenye sherehe. Ili kumweka mke wake nyumbani, Muyaka anatumia ujanja fulani. Anampa mke wake kazi ngumu ambayo itamchukua muda na pia itamtia doa ambalo litamzuia kujumuika na wake wenzake katika sherehe hiyo ya ndoa. Mtunzi anamtaka mke wake katika maelezo ya ubeti wa 1 afanye yafuatayo:

Nipatia kiberiti na mrututu kashobo
Atie mtanashati fumo la kiriborobo;
Yu hapo hana bahati, tubu mwana
wa kabobo;
Hu shuka huna urobo, utavaa nguo
gani?

Kazi hiyo anayompa mke wake ni ya kupaka sumu ya kiberiti na dawa ya mrututu katika mkuki wake mkali, wa usasi. Kwamba Muyaka alijihusisha na shughuli za usasi katika maisha yake, inathibitishwa na maelezo ya shairi lake la 'Ndimi Muinda' ambalo limerejelewa hapo awali. Mkuki huo pia, unaweza kuwa wa vita, kwani Muyaka katika mashairi yake ya siasa ameonyesha kuwa mji wake wa Mombasa ulipigana vita dhidi ya maadui. Muyaka alishiriki katika vita hivyo. Anasema katika mojawapo wa beti za shairi juu ya vita, kuwa:

Jifungetoni masombo mshike msu na
ngao!

Zile ndizo zao sambo, zijile zatoka
kwao;
Natuwakalie kombo tuwapige hario!
Wakija tuteze nao, wayawiapo
ngomani.

Itakuwaje mwanamke aushike mkuki wa vita au hata wa usasi, ilhali kwa kawaida, hii huwa kazi ya wanaume? Hali hii ndiyo inayoonyesha kuwa azma ya Muyaka katika kumtaka mke wake afanye kazi ambayo haikutengewa wanawake, inahitaji kushukiwa. Kwa maelezo ya Abdulaziz (1979: 280), sumu ya kiberiti hutoa harufu mbaya sana. Sumu hii ikiguswa, harufu yake hubakia mkononi kwa muda mrefu mno. Muyaka anapomwambia mke wake amfanyie kazi hii, anajua sawasawa athari za kuishika sumu hiyo. Muyaka anatarajia kwamba, iwapo mke wake ataamua kwenda katika sherehe hiyo, hakuna mtu atakayemkaribia, kwa sababu ya harufu hiyo mbaya. Kwa hivyo, ombi lake kwa mke wake ni la maksudi. Aidha, hii ndiyo sababu inayomwelekeza kumwambia kuwa, “Yu hapo hana bahati, tubu mwana wa kabobo”. Bahati yake ni mbaya kwa sababu, licha ya kuwa ‘mtanashati’, mke mwenye urembo mwingi, ‘wa kabobo’, kama anavyomwita, hawezi kijiunga na wenzake katika sherehe.

Muyaka anampuuza mke wake. Upuuzaji huu ni wa kujaribu kumfanya mke wake aamini kuwa amekuwa si mrembo tena wa kuweza kwenda katika sherehe. Furaha ya Muyaka ni kwamba, anafahamu vyema kuwa mke wake hawezi kwenda kwenye sherehe bila nguo mpya, au nzee pia, lakini maridadi. Muyaka hana shaka na mawazo yake kwa sababu, hii ni desturi ya wake wa Kiswahili wanaokwenda katika sherehe zao za arusi! Hii ndiyo sababu inayomfanya Muyaka azungumzie jambo hili kwa kejeli. Anasema, “Hu shuka huna urobo! Utavaa nguo gani?” Urobo ni kipande cha nguo. Kwa maana hii, Muyaka anaonyesha kuwa mke wake hana nguo yoyote ya maana ambayo anaweza kuvaa kwa minajili ya sherehe hiyo. Hii ndiyo silaha yake ya kumfungia mke wake nyumbani. Jamii ya Waswahili imempa mume katika ndoa jukumu la kumtunza mke na watoto wake, kwa kila hali (Wandera, 1996). Mume ndiye wa kumvisha, kumlisha na kumwongoza mke wake. Maadamu mume anajiweza, ni sharti amtimize mke mahitaji yake yote. Kwa hivyo, waume Waswahili hujitahidi kwa kila namna ili watimize majukumu yao. Wake hutunzwa kwa mavazi mazuri na mapya mara

kwa mara hasa panapokuwa ana sherehe kama vile, ya harusi. Hakuna mume ambaye hupenda kuwa na mke asiye nadhifu kwa mavazi na afya ya mwili, chambilecho Waswahili wenyewe, “mke ni nguo”. Muyaka anaonekana kuitumia nafasi yake ya kuwa mwenye kukimu mahitaji ya mke wake, kama silaha fulani ya kumzindua mke wake juu ya tabia yake fulani ambayo haikumfurahisha, kama itakavyoonyeshwa baadaye.

Katika ubeti wa 2, Muyaka anapambanua zaidi swala la mke wake kutokuwa na nguo ya kumwezesha kwenda kushereheke na wenzake. Mtunzi anaonyesha hali hii kwa mzaha. Anamtolea mifano ya mavazi duni ambayo anamnasihia ayavae ili aende harusini. Ubeti unaelezea:

Ka'ta tene la mkeka au domo la
kanda,
Hadharani ukifika usikalie kit'anda
Wenzio watakuteka utamani la
kutenda:
Kesho wenzio washinda, utavaa
nguo gani?

Muyaka anamwelezea mke wake kuwa, kwa vile hana nguo ya sherehe, akate kipande cha mkeka au kile cha mfuko wa kuwekea vyakula unaosukwa kwa miyaa ili avae akienda katika sherehe. Inaelekea kwamba, hii ni stihizai kwani, itakuwaje mahluki anayevaa nguo ageuke na kuwa wakuvaa vipande vya mkeka au kanda. Muyaka anasema mambo haya kwa maksudi. Anachotaka Muyaka, ni mke wake kuchekwa ikiwa atahiari kwenda kwenye sherehe hiyo. Anamwambia, “Hadharani ukienda usikalie kitanda”, nia yake ni kuwa mke wake akalie kiti ndipo kila atakayehudhuria sherehe aweze kumuona bila shida. Kwa kweli, yeyote atakayemuona katika hali hiyo, atamcheka asijue la kutenda. Raha ya kutaka mke wake afedheheke mbele ya watu sharti iwe ina sababu maalumu. Itakuwaje mume mwenye heshima zake amtake mke wake achekwe!

Maelezo ya ubeti wa 3 yanatoa sababu za Muyaka kumtendea mke wake maovu hayo. Mtunzi anaonyesha kuwa, mke wake ni mkaidi na hana heshima kwake. Huenda hii ndiyo sababu inayomwelekeza mtunzi kumnyima mke wake nguo mpya, Pamoja na ruhusa ya kutoka licha ya kutaka

kumfedhehesha hadharani. Muyaka anadai katika ubeti huu, ya kwamba:

Nalikwambia “sitende”, ukaniambia
“T’atenda!”
Iwe mwana usenende, ukanambia
“T’akwenda”
Leo u mavundevunde ufuamile
kitanda.
Kesho wenzio washinda, utavaa
nguo gani?

Kutokana na maelezo haya, huenda Muyaka na mke wake wamepata kukorofishana. Mtunzi anaonyesha kwamba, amewahi kumkanya mke wake asifanye mambo fulani lakini mke wake akampuuza. Kwa hivyo, hatua ya kumnyima mke wake ruhusa ya kutoka na kutomnunulia nguo ni malipo yake kwa mke wake kwa kuwa mtovu wa heshima chambilecho wahenga, “mwana mkaidi hufaidi siku ya Idi.” Kurani inamshauri mume kumwadhibu mke mkaidi katika sura ya 4 aya ya 34 kwa kusema:

Na wanawake ambao mnaona uasi
wao kwenu
Waonyeni na waacheni peke yao
katika vitanda
Na wapigeni. Na kama wanakutiini
msiwatafutie
Njia (ya kuwaaudhi bure). Hakika
Mwenyezi
Mungu ndiye aliye juu ya Mkuu.

Lakini, wanasheria Waislamu na hata mafundisho mengi ya Mtume Muhammad, yanawahimiza wanaume Waislamu dhidi ya kuwapiga wake wao. Hata hivyo, Doi (1994: 40) anasema kuwa, wakati mwingine adhabu ya kumpiga mke pasipo kumdhuru huhitajika. Msomi huyu anathibitisha dai lake kwa kusema kuwa, mtume mwenyewe aliruhusu adhabu ya kumpiga mke pale ambapo mume aliepukana na kumpiga mke wake usoni au kumpa alama yoyote katika sehemu yoyote ya mwili wake. Ili kumfunza mke wake adabu, Muyaka ameitumia fursa hii ya kwenda katika sherehe kama silaha maalum. Silaha hii inaonekana kufua dafu kwani, mke wake amebaki kifulama kitandani huku amevunjika moyo, kwa sababu ya kukosa nguo na ruhusa ya kutoka nyumbani. Mtunzi anaelezea hali ya mke wake kwa kusema, “leo

u mavundevunde ufuamile kitanda”. Muyaka basi, anamdhibitishia mke wake kuwa, ‘mpiga ngumi ukutani, humiza mkonowe’.

Moyo wa kisasi kwa mke wake unazidi kuonekana katika ubeti wa 4. Muyaka anamnasihia mke wake atumie mavazi duni zaidi iwapo ni lazima aende katika sherehe. Mavazi haya si ya kukubalika fauka ya kwamba hayana heshima. Mtunzi anamwelekeza mke wake kuwa:

Pata tambaa la jaa ujifunge la
uwinda,
Wenzio watashangaa harusini
uchenenda:
Itakupata naza mara hiyo utakonda
Kesho wenzio washinda, utavaa
nguo gani?

Muyaka anamwambia mke wake atumie kitambaa cha kuokotwa jaani. La ajabu ni kwamba, anahitajika ajifunge kitambaa hicho kama winda. Inakadiriwa kuwa, matumizi ya lugha hii kali kwa mke wake, imetokana na yale anayoyalalamikia katika ubeti wa 3. Muyaka ana ghadhabu kwa sababu ya kutosikizwa na mke wake. Hii ndio hasira inayojitokeza katika ubeti wa 4. Kwa kawaida, haitarajiwi mtu mzima kumwambia mwenzake ajifunge nepi kama mtoto mchanga! Muyaka anatumia maneno haya makali ili kuavya muye. Ndio maana anamtahadharisha mke wake kwamba, afahamu kuwa akienda katika sherehe, huku amejifunga ubinda, aibu itampata kiasi cha kumkondesha mara moja.

Shairi la ‘Utavaa nguo gani?’, linatoa maelezo bayana juu ya mke anayemkosea mume wke heshima na, pia, linabainisha athari ya kitendo hicho. Muyaka anaonyesha kuwa, katika jamii yake, inayomtwika mume mzigo wa kuiongoza familia yake, mke wa aina hii hana budi kudhurika kwani, aghalabu, maisha huwa ni nipe nikupe, yaani mtendee mwenzako unavyotarajia akutendee. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba kila mhusika katika ndoa ajue wajibu wake na ajitahidi kuutumiza. Katika kutoa kalima juu ya picha ya mwanamke inayojitokeza katika shairi, sharti asili ya tukio linaloelezwa lizingatiwe kwa makini.

Katika ubeti wa 3, mke anaonekana kuwa ndiye anayemwingiza mume wake katika kumtendea ubaya

huo wote. Mume hakumnyima mke wake nguo au ruhusa ya kutoka, kwa sababu ni mazoea yake kufanya hivyo. Mume amekosa kumpa mke wake vitu hivyo kwa vile mke huyo hana heshima. Kawaida, anayekosa huadhibiwa. Mume ana haki ya kumuadhibu mke wake kiasi cha kumpiga, mradi tu asimuumize wala asimpige kwenye uso. Kwa hivyo, hali hii ni sharti ieleweke kama mfano wa kwenda dukani kununua bidhaa. Mwenye duka atakupa bidhaa uitakayo ikiwa nawe utampa pesa zinazoweza kugharamia bidhaa hiyo. Bila pesa, huwezi kupewa bidhaa. Mke asiye na nidhamu na heshima kwa mume wake, vivyo hivyo, hana budi kutofaidi kutoka kwake. Muyaka anapomnyima mke wake ruhusa ya kutoka, na vile vile, nguo ya sherehe, haimaanishi kuwa anamchukia.

Ilivyoonyeshwa katika maelezo ya ubeti wa 1, Muyaka amemtaja mke wake kama mrembo na mwenye haiba ya uzuri kama walivyo wanawake wenzake. Kwa hivyo, si kweli kwamba mtunzi hampendi mke wake, isipokuwa anajaribu kurekebisha tabia ya mke huyo kwa kumwadhibu. Mke ana haki yake ya kindoa ya kudai kununuliwa nguo. Anapodaiwa, mume anawajibika kutekeleza dai hili isipokuwa ikiwa mke mwenyewe ana makosa, kama vile utovu wa heshima. Hali hii inaongozwa na shuruti kuwa heri mume akamilishe jukumu lake la kumrudi mke wake hapa duniani kuliko kungojea akhera kwenda amua kuwa mke atupiliwe motoni, kama Mwanakupona anavyodokeza katika utenzi wake!

Shairi: Kuonana na Wewe

Fumbo la Ninga

Katika shairi hii la mapeenzi, Muyaka anazungumzia hali mbalimbali za uhusiano wake na mpenzi wake. Mtunzi anaonyesha jinsi imekuwa vigumu kwake kukutana au hata kumwona mpenzi wake. Sababu kuu ya ugumu huu ni kuwa, msichana ametawishwa. Muyaka anaelezea kuwa, hana njia ya kukutana na msichana huyo au hata kumtuma mjumbe. Msichana huyo amechungwa barabara. Kwa sababu hii, Muyaka amebaki kuwazia mbinu mpya atakayotumia ili aweze kuonana na mpenzi wake, kwani kwa sasa hakuna upenyenye wowote anaoweza kuutumia kumwona binti huyu. Muyaka anaeleza katika ubeti wa 1:

Kwamba risala afika, mjumbe wa
Ko'ngowea,

Angekuja na waraka mwema
akakuletea,
Au angelitamka maneno
akakwambia,
Lakini hapana ndia ya kuonana na
wewe.

Huo ndio uhalisi unaojitokeza katika jamii ya Waswahili (Wandera, 1996). Kwamba wasichana wa Kiswahili wa tabaka la juu, walitawishwa ili wasiweze kuonana na mtu yeyote asiye na uhusiano wa karibu na wao. Mtunzi anaonekana amejiuzulu kumuona huyo msichana. Tamaa yake sasa ni kuwa mjumbe ampelekee risala kwa msichana huyo. Jambo hili pia haliwezekani, kwa vile hakuna njia yoyote inayoweza kupitiwa ili kumfikia msichana huyo.

Ubeti wa 2 unaonyesha kuwa, mtunzi amemaliza muda mrefu bila kumuona msichana huyo. Muyaka anakariri kuwa:

Lakini Hapana ndia ya Muwanga ilo
wazi,
Ndipo akalimatia kuja kwako
matembezi,
Penyenye ya kupenyea siioni kwa
maozi,
Ndipo hafanya ajizi ya kuonana na
wewe:

Sababu ya kumaliza muda mrefu bila ya kuonana kwa hawa wapenzi ni hiyo hali ya kutawishwa kwa msichana. Kwa kuwa Muyaka amejaribu kila njia na akakosa kupata uwezekano wa kumuona msichana, ameamua asimtembelee tena. Kwa hivyo, ugumu huu ndio umemtia Muyaka uvivu wa kutembea.

Katika ubeti wa 3, jitihada zote zinazotumiwa katika kumtawisha msichana huyo zinajitokeza. Kila njia inayoingia kwa akina msichana imewekewa walinzi! Walinzi hawa wameajiriwa kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote anayeingia huko bila idhini ya wazazi wa binti huyo. Hawa ndio watu anawaogopa mtunzi kwani anasema:

Ndipo hafanya ajizi
ningelikutokeleza,
Pasi kuona manyezi hatakasa yangu
niya,
Ela nawacha walinzi walindao kulla
mwiya,

Ndipo hajizulia nisionane na wewe.

Walinzi hawa wamemfanya Muyaka aingiwe na uoga, pamoja na uvivu wa kujaribu angalau kupata upenyepenyepye wa kumfikia msichana.

Katika ubeti wa 4, Muyaka anaonyesha ukinzano na mawazo juu ya hatua anayoweza kuchukua ili asuluhishe hali yake na mpenzi wake. Huenda, mojawapo ya yale yanayomkabili akilini ni kupuuzwa walinzi na kujikakamua ili aende kumuona msichana. Ukinzano wake wa mawazo anaueleza kwa kusema:

Ndipo hajizulia, moyo unгатоaweza,
Kinyume haushikia, kisha
nikauliwaza,
Nisiche kuukemea kwani upate
punguza,
Kwa kukosa muwangaza wa
kuonana na wewe.

Muyaka anasema kuwa, hali hii ngumu ya kujisaili kimawazo, imemtuliza moyo. Kitendo hiki basi kimemwezesha kukubali hali hii ya kuzuiwa kuonana na mpenzi wake.

Maelezo ya ubeti wa 5 vilevile yanazidi kuonyesha mtunzi akisaili nafsi yake. Anachotaka ni kupata utulivu wa mawazo. Anaelezea kuwa, kushindwa kwake kupata suluhisho la tatizo ambalo analo, ni mithili ya mtu anayeshindwa kuona hata pale penye muwangaza wa kutosha. Hali yake tatanishi imemfanya kuwa kipofu. Anaona giza pekee. Kwa mwelekeo huu, Muyaka hana njia ya kumwezesha kupata jawabu. Ubeti unanakiri:

Kwa kukosa muwangaza muwanga
ungazagaa,
Huona kikuu kiza nilipo nikiangaa
Usambe vyanipendeza kwa hilo
sikukataa!
Napenda sikuliwaa la kuonana na
wewe.

Ingawa Muyaka ameshindwa kumuona mchumba wake, anamfahamisha kupitia kwa risala kuwa asidhani kwamba, anafurahia hali hii kwani amefanya kila juhudi kuiondoa lakini hakufua dafu. Mtunzi anaonyesha kuwa, amewahi kukutana na binti huyo hapo awali. Huenda ikawa hiki ndicho kichocheo cha hamu yake

kubwa ya kutaka kumuona msichana huyo kwa mara nyingine.

Kuanzia ubeti wa 6 hadi wa 9, ambao ni ubeti wa mwisho, Muyaka anazingatia kudhihirisha sifa mbali mbali za msichana huyo. Katika ubeti wa 6, anaelezea sababu zinazomfanya ampende msichana huyo. Mtunzi anamwambia msichana:

Napenda sikuliwaa, mwandani
wangu mpenzi,
Kwa wema ulinitwaa kwa huruma na
mbawazi.
Huwaje kukuwambaa, kwa leo,
nyakati hizi?
T'afanyaje makatazi ya kuoana na
wewe?

Muyaka anamsifu msichana kwa takriri ya "Mwandani wangu mpenzi". Hii inaonyesha jinsi mtunzi anavyompenda msichana huyo. Msichana huyo anaelezwa kuwa mwenye utu na moyo wa huruma. Muyaka anadai kuwa, msichana huyo amemtwa. Matumizi ya neno 'twaa' yanaleta maana ya Muyaka kuwa na urafiki mkubwa na huyo msichana. Maadamu, kutwaa kitu ni kukitoa kitu mahali kilipo na kukiweka au kukishika mkononi. kwa hivyo, Muyaka anadai kuwa mpenzi wake amemuweka mkononi mwake. Hali hii ina maana kuwa mpenzi wa Muyaka ndiye anayekidhi mahitaji yote ya mtunzi. Muyaka katika hali hii anajiona kama mwenye bahati ya milele na ndio maana anamwambia msichana huyo kuwa, hawezi kumwepuka au kumhepa hata kama hawaonani! Kwa hivyo, inaelekea kwamba, Muyaka ameamua kuendeleza mapenzi yao kwa sababu ya heshima, utu na imani ya mchumba wake.

Sifa za msichana zinazidi kuonyeshwa katika ubeti wa 7. Muyaka anampamba mpenzi wake kwa jazanda za mwana-ninga na lulu. Katika hali hii, mtunzi analinganisha tabia na sifa za msichana huyo na tabia na sifa za hivyo vitu vinavyorejelewa. Muyaka anaeleza:

T'afanyaje makatazi kwako wewe
mwana-ninga?
Ndiwe lulu ya mvazi, ipendezao
kutunga!
Ikapangua simanzi zamani na
kujifunga.

Kukuata ni ujinga, kutoonana na wewe.

Jazanda hizi, zinadhihirisha kuwa msichana huyo ana sifa mbalimbali zinazomvutia Muyaka. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifi, ninga ni ndege mdogo wa jamii ya tetere mwenye rangi ya kijani na miguu miekundu. Ndege huyu anavutia kwa sababu nyingi: rangi yake, ulaini na usafi wa manyoya yake, unene wa kifua (maziwa) chake, sauti yake na macho yake. Kwa hivyo, mtunzi anapomrejelea msichana huyo kwa jina, mwana-ringa, ana maana kuwa, mchumba wake anavutia kwa sababu ya ujana na urembo wake mithili ya mwana-ringa. Pia, kuna uwezekano kuwa, Muyaka anaashiria ugumu wa kumfikia mpenzi wake kwa kuumithilisha na ugumu wa kumfikia mtoto wa ninga. Kwa hivyo, ulinzi anaopewa mchumba wake ni kama ule wa mwana-ninga. Kwa kawaida, ninga si ndege wa kuonwa ovyo ovyo kwa sababu mara nyingi huwa angani. Hali hii ndio inayowaelekeza Waswahili kusema kuwa, “uko juu kwa juu kama ninga”.

Fumbo la Lulu

Kuhusu fumbo la lulu, Inyani (1994: 48) anasema kuwa, mwanamke yeyote anayesifiwa kuwa a lulu, ni yule ambaye ni mrembo asiye na kifani. Kamusi ya Kiswahili Sanifu inaelezea kwamba, lulu ni kitu kama changarawe, cheupe au cheusi kinachong'aa na chapatikana katika chaza. Hutumika kuwa ni kito katika mapambo. Mtunzi anasema kuwa lulu hii humpendeza daima anapoivaa. Aidha, lulu hii inapovaliwa humwondolea mtu huzuni au shida yoyote nyingine aliyo nayo. Kwa hivyo, lulu hii si pambo tu bali pia ina kazi sawa na hirizi. Ilivyoelezwa awali, mume wa Kiswahili hutarajia kumpata mke nadhifu, mwenye heshima na anayejua kumtunza na kumtuliza roho baada ya shughuli za kutafuta riziki. Kama anavyosema Sheikh Saagaf (mhojiwa) wa Mombasa, mke mzuri atamfanya mume wake atake kuwa nyumbani kila mara. Hali hii humwezesha mume kuwa na afya nzuri na isitoshe, humfanya awe nuru kwa wanajamii wengine. Hali hii inaelekeza katika kukubaliana na msemu wa kiingereza unaodai kuwa, mume yeyote anayefaulu maishani, huwa amepata msaada kutoka kwa mke wake. Msaada huo si lazima uwe wa kifedha, unaweza kuwa wa kihali au wa kupewa mawaidha ya busara. Hii ni kwa sababu, iwapo mume ana matatizo na mke wake, hawezi kuwa na

akili tulivu ya kumwezesha kuwazia jambo lolote la manufaa.

Matumizi ya mafumbo haya kwa mwanamke yanasadifu sifa za kawaida alizo nazo mwanamke. Inyani (1994: 72) anasema kuwa, sababu za kutumia mafumbo kama vile ua, lulu, ninga, na njiwa katika kuwaashiria wanawake, katika jamii ya Waswahili zinatokana na hali kwamba, aghalabu wao ni warembo, wana tabia nzuri na wanapenda kusifiwa pia. Ni njia mojawapo ya kuonyesha mapenzi kwao. Kuwalinganisha wanawake na kitu kisicho na uhai au kiumbe kama ndege si njia ya kuwakashifu au kuwagandamiza kama anavyodai Imbosa (1990). La hasha! Kama ilivyooneshwa hapo awali, hii ni njia ya kuwatukuza wanawake, hasa sifa za mifano ya jazanda zinazorejelewa zikitiliwa maanani.

Pamoja na ubeti wa 8 kutoa sifa zaidi za msichana, ubeti huu pia umeonyesha kwamba msichana huyo ni mtoto wa familia bora. Katika jamii iliyozingatia utabaka, maelezo ya mtunzi huyu katika shairi hili yanasadifu aina ya maisha waliyoishi watu wa tabaka la juu. Mathalan, ni watu wa tabaka hili walioweza kuwatawisha barabara wake na watoto wao wa kike ilivyohitajika katika jamii hii, kwa sababu ya mali waliyokuwa nayo. Hii ni kwa vile hali hii ilihitaji pesa zaidi: kwa mfano pesa za kununua vifaa vya kujengea majumba makubwa yenye sakafu juu na kila kitu ndani; pesa za kuwaajiri watumwa wa kufanya kazi zilizohitaji kutoka nje; licha ya zile za kuwalipa walinzi wa kulinda milango na njia za kutoka nje. Hali hii, ndiyo inayobainika katika ubeti wa 3 uliochambuliwa awali. Mtunzi anamwambia mpenzi wake katika ubeti wa 8 kuwa:

Kukuata ni ujinga ambao ni wa milele
Nawe zidi kukitunga cheo chako si
kitule:
Na kule kukibananga, ndiyo haya
niketele,
Usambe linitukile la kuonana na
wewe!

Muyaka anazidi kumtia moyo mpenzi wake kwa kumwelezea kuwa, asitamauke juu ya mapenzi yao kwani yeye daima atampenda. Kwa hivyo, anamnasihhi binti wa watu kuwa asijaribu kujiharibia sifa yake na ya wazazi wake, labda kwa kutaka kuukwepa

utawishwaji. Muyaka anamhakikishia kuwa bado ana imani naye. Jambo la muhimu kwao, ni kuvumilia na kuikubali hali yao kwa vile, mvumilivu hula mbivu.

Kilele cha sifa za msichana kinadhihirishwa katika ubeti wa 9. Muyaka anasisitiza urembo wa msichana huyo fauka ya kuthibitisha kuwa, msichana huyo anatoka katika tabaka la juu. Muyaka anasema:

Usambe linitukile, mtanashati
mrembo!
Mwana wa zilungu – pule, uso t’ua
wala k’ombo!
Mambo mawi sitenzile, ukajandika
misimbo!
Nalipenda lako umbo tuonapo
minawe!

Sifa ya msichana huyo ya kuwa, ‘Mwana wa watu’, inajitokeza katika maelezo ya Abdulaziz (1979: 242) anapofafanua maana ya ‘mwana wa zilungu – pule’. Anasema kuwa maneno haya yana maana ya mwana wa majumba ashirafu, yaani mwana mwenye kuzaliwa katika familia yenye mali. Ndio maana katika kumsifu msichana huyo, Muyaka anasema, “uso t’ua wala kombo”. Hii ina maana kwamba msichana huyo hana ila yoyote katika mwili wake, kama vile kuwa na kiungo cha mwili kilicho kombo. Aidha, hakuna anayetarajia watu wa tabaka la juu kushindwa kuwalisha, kuwavisha na kuwatibu watoto wao vyema wanapoonyesha dalili ya kupata ugonjwa wowote ule! Kwa hivyo, watoto hawa hawana budi kuwa na miili yenye siha na urembo wa kuvutia. Muyaka

amedhihirisha kuwa msichana huyo ana kila sifa za ‘mtoto wa watu’.

Ni dhahiri kuwa, kutokana na maelezo ya shairi la ‘Kuonana na wewe’, mwanamke ametukuzwa kwa kupewa sifa mbali mbali. Sifa hizi, zinasadifu zile sifa ambazo zilisisitizwa katika jamii ya Waswahili ya karne ya kumi na tisa, kama inavyotambulika katika utamaduni wao (Wandera 1996). Kwa hivyo, Muyaka amesawiri picha halisi ya mwanamke wa jamii ya wakati wake.

HITIMISHO

Katika mashairi teule ya Muyaka yaliyohakikiwa, taswira ya mwanamke inayojitokeza ni yenye sura mbalimbali. Kwa kifupi, mwanamke katika jamii ya Waswahili ya wakati wa Muyaka ana sifa za uzuri si wa urembo tu bali pia tabia. Mwanamke aliyechorwa ni yule aliye na uzuri maridhawa, nadhifu, mwenye utu, mama, na mke bora. Yeyote anayetenda kinyume na haya husutwa, kwani huwa mfano mbaya kwa wengine. Ni ‘mtu asiye wa haja’. Muyaka ameonyesha kiasi fulani cha wanawake waliokuwa na sifa zilizosutwa na jamii; kama vile kuwafanyia waume wao ujeuri. Kwa hivyo, taswira ya mwanamke inayochorwa katika mifano ya uhakiki huu imeweza kutoa sifa ambazo mwanamke wa Kiswahili wa karne ya kumi na tisa aliyokuwa nayo. Muyaka amewasilisha sifa hizo sio kwa ujumbe tu bali pia kwa aina ya lugha anayoitumia kuwahuisha wanawake hao. Ametumia mafumbo yanayoainisha bayana sifa za wanawake wa Kiswahili.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka 19th Century: Swahili Popular Poetry*. Kenya Literature Bureau
- Doi, A. R. I. (1994). *Woman in Shariah (Islamic Law)*. Ta-Ha Publishers Ltd.
- Gibbe, A. G. (1995). *Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia*. Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Moi.
- Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Clarendon Press.
- Hichens, W. (1940) *Diwani ya Muyaka Bin Haji Al-Ghassany*. University of Witwatersrand Press
- Imbosa, R. (1990). *Jazanda katika Ushairi wa Muyaka*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Inyani, K. S. (1994). *Sexist Overtones in Kiswahili Women Metaphors: A Critical Analysis*. Makala ya OSSREA.
- Kurani Tukufu. (1974).
- Kurani Tukufu. (1981). Tafsiri ya Kiswahili.
- Magayu, K. M. (1977). East African Literature and the East African Writer. *Journal of East African Literature and Creative arts*.
- Wandera, S. P. (1996). *Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900: Uhalisia au Ugandamizwaji?* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton.